



Mungu Amtuma Musa Nchini Misri

KUTOKA SURU YA 3-12



YEHOVA NDIYE ALIYEKUWA
AKIZUNGUMZA
KUPITIA MALAIKA.



MUSA NA HARUNI NDUGU YAKE,
WAKAONDOKA
ILI WAKUTANE NA FARAO.

YEHOVA ANASEMA:
"WARUHUSU WATU
WANGU
WAENDE ZAO
WAKANITUMIKIE
NYIKANI."

YEHOVA NI NANI?
SITAWARUHUSU
ISRAELI
WAENDE ZAO.

HARUNI ALIFANYA MUUJIZA MBELE YA FARAO ILI
ATHIBITISHE KWAMBA MUNGU NDIYE ALIYEKUWA AMEWATUMA.
(SOMA KUTOKA 7:8-13.)

LAKINI FARAO AKAWA MKAIDI.
HAKUWARUHUSU
WATU WA YEHOVA WAONDOKE MISRI.

YEHOVA AKALETA
MAPIGO TISA KATIKA NCHI
YA MISRI.

ALIYAGEUZA MAJI YA MTO NILE KUWA DAMU.

VYURA WALIFUNIKA NCHI NZIMA.

WADUDU WADOGO
WANAOTIWA
CHAWA WALIWASHAMBULIA
WANADAMU NA WANYAMA.

MAINZI YALIJAA NDANI YA NYUMBA
NA KUJARIBU NCHI.

WANYAMA WENGI WALIUGUA NA KUFU.

WAMISRI NA WANYAMA WAO
WALIUGUA **MAJIPU** YENYE MALENGELENGE
NA MAUMIVU MAKALI.

MOTO NA **MVUA YA MAWE** ILIHARIBU
MASHAMBA
NA KUUA WATU NA WANYAMA.

NZIGE WALIKULA
MIMEA YOTE ILIYOACHWA
NA **MVUA YA MAWE** ILIYOLETA UHARIBIFU.

GIZA LILIFUNIKA
NCHI KWA SIKU TATU.

LICHA YA HILO, FARAO ALIKATAA
KUWARUHUSU WAISRAELI
WAONDOKE.

MUSA NA HARUNI WALIENDA
TENA
KUMWONA FARAO.

YEHOVA AMESEMA:
"NITALETA PIGO
LINGINE MOJA KATIKA NCHI
YA MISRI.
KATIKATI YA USIKU HIVI, KILA
MZALIWA WA KWANZA WA
KIUME
ATAKUFA."

IKAWA HIVYO. USIKU HUO, YEHOVA ALIMTUMA
MALAIKA WAKE NAYE AKAMUUA KILA **MZALIWA WA
KWANZA WA KIUME** KATIKA KILA NYUMBA YA WAMISRI
WALIOKATAA KUMTII MUNGU . . .

ALIMUUA HATA **MWANA WA
FARAO**. (SOMA ZABURI 78:
49-51.)

SIMAMENI,
MWENDE,
MKAMTUMIKIE
YEHOVA, KAMA
MLIVYOSEMA.

HATIMAYE WAISRAELI WOTE
WAKARUHUSIWA **KUONDOKA MISRI**.

LAKINI BADO WALIKUWA WAKIKABILI
HATARI FULANI. YEHOVA **ALIWALINDA** JINSI GANI?
HADITHI ITAKAYOFUATA ITAJIBU SWALI HILO.

TUNAJIFUNZA NINI KUTOKANA NA HADITHI HII?

KWA NINI FARAO **HAKUWASIKILIZA** MUSA
NA HARUNI?

DOKEZO: KUTOKA 9:17; ZABURI 66:6, 7.

TAJA **TOFAUTI** KATI YA MUSA NA
FARAO?

DOKEZO: HESABU 12:3.

KWA NINI UNAFIKIRI NI VIZURI KUWA
MPOLE BADALA YA KUWA MKAIDI NA MWENYE
KIBURI?

DOKEZO: ZABURI 37:11; ZEKARIA 7:8-12.